SUMBAWANGA CATHOLIC DIOCESE
PREVENT and CURE
Diocesan Health Board

**KUMB NA. NDDH/VA/ 01/ 2025/ 02** **25 MACHI,2025.**

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.

### 1.UTANGULIZI.

Jimbo Katoliki Sumbawanga linapenda kutangaza nafasi za kazi za Mkataba wa Kujitolea na Mkataba wa ajira katika fani mbalimbali za kada ya Afya na zisizo za Afya.

Jimbo linatangaza nafasi Kufanya kazi katika ***Hospitali Teule ya Wilaya Nkasi (NDDH)*** *na* ***Taasisi ya Mafunzo ya Afya ya Mt.Bakhita.*** Taasisi hizi zinazopatikana katika Mji wa Namanyere Wilaya ya Nkasi Mkoani RUKWA.

Hivyo,Jimbo Katoliki Sumbawanga linapenda kuwajulisha Wananchi wenye sifa na vigezo kuomba kazi katika nafasi tajwa hapo chini:-

| **KITUO CHA KAZI:**<br>**HOSPITALI TEULE YA WILAYA NKASI (NDDH).** | | | |
|---|---|---|---|
| **NA.** | **KADA** | **KAZI NA MAJUKUMU** | **MASHARTI YA AJIRA** |
| 1 | **Afisa Muuguzi Msaidizi Daraja la II.**<br>**(Nafasi -4)**<br>**ELIMU.**<br>Elimu ya Stashahada ya Uuguzi na Ukunga (Diploma in Nursing and Midwifery)<br>Muombaji aliye na Stashahada ya juu atapewa kupaumbele (Advanced diploma). | (i) Kutoa huduma za Uuguzi.<br>(ii) Kukusanya Takwimu Muhimu za Afya<br>(iii) Kuwaelekeza kazi waunguzi walio chini yake<br>(iv) Kuelimisha Wagonjwa na Jamii kuhusu matatizo yao ya kiafya.<br>(v) Kutoa huduma za Kinga na Uzazi<br>(vi) Kufundisha Wanafunzi katika Chuo cha Mafunzo ya Afya ya Mt.Bakhita.<br>(vii) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, Uzoefu na ujuzi wake. | Kujitolea,Mkataba wa Mwaka 1. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 2 | **Daktari Daraja II.**<br>**(Nafasi 1).**<br><br>**ELIMU.**<br>**Shahada ya Udaktari (Doctor of Medicine)** | (i) Kufanya kazi zote za matibabu Hospitalini.<br>(ii) Kutoa na kusimamia elimu ya Afya Kituoni.<br>(iii) Kutunza takwimu na kuzitumia.<br>(iv) Kupanga na kutathimini huduma za afya.<br>(v) Kufundisha wanafunzi katika Chuo cha Mafunzo ya Afya ya **Mt.Bakhita.**<br>(vi) Kusimamia na kuelekeza wafanyakazi walio chini yake<br>(vii) Kubuni na kuendesha utafiti na kusambaza matokeo<br>(viii) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, Uzoefu na ujuzi wake. | Kujitolea,Mkataba wa Mwaka 1 |
| 3 | Mtaalamu wa Maabara II (Laboratory Scientist) - **Nafasi 1**<br><br>**<u>ELIMU.</u>**<br>Shahada ya Maabara za Binadamu (BSC. in Medical Laboratory.) | (i) Kufanya uchunguzi wa kimaabara katika na utafiti (Research laboratories);<br>(ii) Kufundisha wanafunzi katika Chuo cha Mafunzo ya Afya ya Mt.Bakhita,<br>(iii) Kuweka Kumbukumbu za matokeo ya vipimo katika rejesta;<br>(iv) Kutunza vifaa na Vitendea kazi vya Maabara<br>(v) Kutoa tafsiri ya matokeo ya vipimo vya maabara.<br>(vi) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake. | Kuajiriwa kwa Mkataba mwaka 1 |

| KITUO CHA KAZI<br>TAASISI YA MAFUNZO YA AFYA YA MT. BAKHITA (ST. BAKHITA HTI- NAMANYERE NKASI. ) | | | |
|---|---|---|---|
| | KADA ZA AFYA | KAZI NA MAJUKUMU | |
| 1 | **Mwalimu -Idara ya Uuguzi na Ukunga** (Tutor Nursing and Midwifery)- **(Nafasi 2)**<br><br>**<u>ELIMU</u>**<br>Shahada ya Sanyasi ya Uuguzi na Ukunga (Bsc. in Nursing and Midwifery/Nursing Education).<br><br>**<u>UFAULU.</u>**<br>3.8 GPA. | (i) Kufundisha wanafunzi katika program husika na nyingine pale inapohitajika<br>(ii) Kutayarisha vipindi vya madarasani<br>(iii) Kusimamia mafunzo kwa vitendo (Field Practices na Clinical rotation kwa wanafunzi).<br>(iv) Kushiriki katika Tafiti mbalimbali (Research) na Ushauri Consultancy)<br>(v) **Kufanya kazi katika Hospitali Teule ya Wilaya Nkasi NDDH**<br>(vi) Kuwa tayari kutumia Mfumo wa Taasisi katika masuala ya kitaaluma na kiutawala.<br>(vii) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, Uzoefu na ujuzi wake. | Kujitolea,Mkataba wa Mwaka.1 |
| 2 | **Mwalimu -Idara ya Utabibu** (Tutor Clinical Medicine)-**Nafasi 2**<br><br>**<u>ELIMU</u>**<br>Shahada ya Udaktari (Doctor of Medicine).<br><br>**<u>UFAULU.</u>**<br>3.5GPA | (i) Kufundisha wanafunzi katika program husika na nyingine pale inapohitajika<br>(ii) Kutayarisha vipindi vya madarasani<br>(iii) **Kufanya kazi katika Hospitali Teule ya Wilaya Nkasi NDDH**<br>(iv) Kusimamia mafunzo kwa vitendo (Field Practices na Clinical rotation kwa wanafunzi).<br>(v) Kushiriki katika Tafiti mbalimbali (Research) na Ushauri Consultancy)<br>(vi) Kuwa tayari kutumia Mfumo wa Taasisi katika masuala ya kitaaluma na kiutawala.<br>(vii) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, Uzoefu na ujuzi wake. | Kujitolea,Mkataba wa Mwaka 1 |
| 3 | **Mwalimu -Idara ya Ufundi Sanifu Maabara.**<br>(Tutor Medical Laboratory).<br><u>NAFASI</u> – **1.**<br><br>**<u>ELIMU.</u>** | i. Kufundisha wanafunzi katika program husika na nyingine pale inapohitajika<br>ii. Kutayarisha vipindi vya madarasani<br>iii. **Kufanya kazi katika Hospitali Teule ya Wilaya Nkasi NDDH** | Kujitolea,Mkataba wa Mwaka 1. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Shahada ya Maabara za Binadamu (BSC. in Medical Laboratory.)<br><br>**UFAULU.**<br>3.5 GPA. | iv. Kusimamia mafunzo kwa vitendo (Field Practices na Clinical rotation kwa wanafunzi).<br>v. Kushiriki katika Tafiti mbalimbali (Research) na Ushauri Consultancy)<br>vi. Kuwa tayari kutumia Mfumo wa Taasisi katika masuala ya kitaaluma na kiutawala.<br>vii. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, Uzoefu na ujuzi wake. | |
| | ***KADA ZISIZO ZA AFYA*** | **KAZI NA MAJUKUMU** | **MASHARTI YA AJIRA** |
| **1** | **NAFASI -1.**<br>MKUTUBI (Librarian)<br><br>**ELIMU.**<br>**Stashahada ya Ukutubi na utunzaji Kumbukumbu** (Diploma in Library and Information Management).<br><br>**UZOEFU.**<br>• Uzoefu usiopungua miaka miwili (2) katika nafasi husika<br>• Aliyefanya kazi katika Taasisi za Elimu atapewa kipaumbele. | i. Kutekeleza majukumu yote ya kimuundo ya Mkutubi sawa sawa ana Miongozo.<br>ii. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, Uzoefu na ujuzi wake. | Kuajiriwa kwa Mkataba wa Ajira. |
| **2** | **Katibu Mhutasi. (Office Secretary) -(Nafasi1)**<br>• Uzoefu usiopungua miaka miwili (2) katika nafasi husika.<br>• Aliyefanya kazi katika Taasisi za Elimu atapewa kipaumbele. | i. Kutekeleza majukumu yote ya kimuundo ya Katibu Mhutasi sawa sawa na Miongozo.<br>ii. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, Uzoefu na ujuzi wake. | Kuajiriwa kwa Mkataba wa Ajira. |

## SIFA ZA JUMLA KWA KADA ZA AFYA.

I. Cheti cha Taaluma kwa Kada aliyosomea cha Chuo kinachotambuliwa na Serikali.
II. Awe amemaliza mafunzo ya kazi(Internship) kwa kada za Udaktari,Maabara na Afisa Muuguzi.
III. Awe amesajiliwa na Baraza la Kitaaluma kwa Kada za Afya.
IV. Awe na Leseni ya Taaluma husika.

## MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI.

Waombaji wote wanatakiwa kuwa na sifa za jumla kama ifuatavyo: -

I. Awe raia wa Tanzania.
II. Awe na umri usiozidi miaka 45.
III. Awe navyeti kamili vya mafunzo ya fani aliyosomea (Cheti cha kidato cha Nne,Sita,Taaluma na Usajili kamili)``Full Registration`` au Leseni hai ya kufanya kazi ya taaluma husika
IV. Maombi yaambatane na wasifu wa mwombaji (CV).
V. Maombi yaambatishwe nakala za vyeti vya Elimu,Taaluma na Cheti cha kuzaliwa.
VI. Testimonials result slip **HAITAKUBALIWA.**

## MSHAHARA.

Malipo ya mshahara yatazingatia Mwongozo wa Afya wa Taifa wa kujitolea wa Julai 2021(National Health workers Volunteering Guideline).

## NAMNA YA KUTUMA MAOMBI.

**Muombaji aandike barua ya maombi ya kazi kwa Anuani:-**

MTAWALA,
HOSPITALI TEULE YA WILAYA NKASI (NDDH.)
S.L.P 17,
**NAMANYERE- NKASI.**

**KUTUMA KUPITIA.**
**Barua Pepe: E. mail: *namanyereddh@yahoo.com.***

**MAOMBI YATAKAYOWASILISHWA KWA NJIA YA MKONO HAYATOPOKELEWA.**

***MWISHO WA KUPOKEA MAOMBI KWA NAFASI ZOTE NI KABLA AU KUFIKA 08/04/2025, SAA TISA NA NUSU ALASIRI.***

Imetolewa na

**PD. COSMAS MAKASI.**
**MTAWALA.**